

TANGAZO LA SERIKALI NA. 405 la tarehe 24/5/2024

SHERIA YA USAFIRI MAJINI,
(SURA YA 165)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 157)

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA USAFIRI MAJINI ZA UCHUNGUZI WA
AFYA ZA MWAKA 2024

- Jina
TS Na.
336 la
2023
1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Usafiri Majini za Uchunguzi wa Afya za Mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Usafiri Majini za Uchunguzi wa Afya za Mwaka 2023 ambazo hapa zitarejewa kama “Kanuni kuu”.
- Marekebis
ho ya
kanuni ya
3
2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kufuta tafsiri ya neno “daktari mwamuzi” na badala yake kuweka tafsiri ifuatayo:
“daktari mwamuzi” maana yake ni daktari mwenye uzoefu husika na ameidhinishwa kwa mujibu wa kanuni ya 4, baada ya Msajili kupeleka ombi la uteuzi wa daktari huyo kwa chombo husika cha ithibati ya matibabu, kwa dhumuni la kufanya mapitio ya matokeo ya uchunguzi wa afya kwa baharia au nahodha kwa mujibu wa Kanuni za Kushughulikia Malalamiko;”.
- TS.Na.
338 la
2018
3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 5(1) kwa-
(a) kufuta aya (c); na
(b) kubadili mpangilio wa aya (d) na (e) kuwa aya (c) na (d) mtawalia.
- Marekebis
ho ya
kanuni ya
18
4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 18 kwa kufuta kanuni ndogo ya (2) na badala yake kuweka ifuatayo:

“(2) Mfumo wa Viwango vya Ubora utaweka taratibu za chini kwa-

- (a) utoaji wa vyeti vya matibabu;
- (b) uteuzi wa daktari; na
- (c) mapitio ya uamuzi wa Shirika.”.

Marekebis
ho ya
kanuni ya
21

5. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 21 na badala yake kuweka kifuatacho:

“Ushughuli
kiaji wa
malalamiko

TS Na.
338 la 2018

21. Baharia au nahodha ambaye hajaridhishwa na maamuzi ya Shirika yaliyotolewa chini ya Kanuni hizi, au kitendo cha mtu mwingine, anaweza kutafuta haki kwa mujibu wa Kanuni za Kushughulikia Malalamiko.”

Kufutwa
kwa
Jedwali la
Tatu

6. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta Jedwali la Tatu.

Dodoma,
3 Mei, 2024

MAKAME M. MBARAWA
Wazairi wa Uchukuzi